Njinga & Sepé: Revista Internacional de Culturas, Línguas Africanas e Brasileiras
São Francisco do Conde (BA) | vol. 5, nº Especial II | p. 65-79 | jul./dez.2025.

# Semi za Kiswahili kuhusu Viungo vya Mwili na Nafasi yake kwa Jamii

**Shani Omari MCHEPANGE** *

ORCID iD https://orcid.org/0009-0007-6910-2194

**IKISIRI**

Semi za Kiswahili ni utanzu muhimu wa fasihi simulizi unaotumika katika mazungumzo ya kila siku miongoni mwa wanajamii. Kutokana na umuhimu wake, semi hizo husawiri masuala mbalimbali ikiwemo viungo vya mwili. Katika lugha ya Kiswahili kuna semi kama vile methali, misemo, misimu, vitendawili na nahau zinazosawiri viungo vya mwili. Hata hivyo, kunakosekana utafiti wa kutosha unaohusiana na uga huu. Ukosefu wa maarifa ya aina hiyo umepelekea kushindwa kufahamu vizuri maudhui na dhima za semi hizo katika jamii. Makala hii inalenga kujibu maswali mawili, swali la kwanza, semi zinazosawiri viungo vya mwili zinazungumzia mambo gani? Swali la pili, semi hizo zina dhima gani kwa jamii husika? Data za utafiti huu zilikusanywa kwa njia ya usomaji wa nyaraka mbalimbali kuhusu semi katika machapisho kutoka maktabani na mtandaoni. Utafiti umebaini kwamba semi hizo zimesheheni maudhui anuwai. Miongoni mwa maudhui hayo ni umuhimu wa viungo hivyo, ufanyaji kazi, umoja na ushirikiano, heshima, tabia njema, malezi na kutunza siri. Maudhui mengine ni kifo, mapenzi, uangalifu na umakini katika masuala mbalimbali. Aidha, imebainika kwamba semi hizo zina dhima mbalimbali ikiwemo kuelimisha, kuendeleza falsafa ya Kiafrika, kuishauri na kuikinga jamii dhidi ya hatari na matatizo mbalimbali.

## Utangulizi

Semi ni utanzu wa fasihi simulizi unaodhihirika katika jamii mbalimbali duniani. Kwa mujibu wa Mauya (2008) semi ni maneno ambayo hupangwa kwa pamoja kisanii na kuleta maana isiyo ya kawaida. Vilevile, inaelezwa na Bianco na Emig (2009) kwamba semi ni maelezo mafupi yanayoonesha uzoefu wa binadamu yanayotumia mtindo maalumu ambao ni rahisi kukumbukika na unaovutia kusikia, lengo lake la msingi ni kuwasilisha kifasihi uzoefu wa mtu kwa wengine. Nao King'ei na Ndalu (2016) wanaeleza kuwa semi ni neno ama fungu fupi la maneno yenye maana fiche linalotumiwa kutoa maadili kwa jamii. Utanzu wa semi huundwa na vipera kama methali, misemo, nahau, vitendawili, misimu/misimo, na shirikina. Hata hivyo, kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia, katika ulimwengu wa sasa, semi hizo hazipatikani tu katika matini simulizi bali pia katika maandishi na mtandaoni. Semi, kama tanzu nyingine za fasihi, huchota maudhui yake katika mazingira ya jamii husika. Mojawapo ya mazingira hayo ni binadamu au wanyama ambao huundwa kwa viungo mbalimbali vya mwili. Viungo hivyo ni pamoja na kichwa, macho, pua, masikio, tumbo, mikono na miguu. Takribani viungo vyote vya mwili vinatumika katika kuunda semi za Kiswahili katika kusawiri masuala mbalimbali katika jamii. Kwa mfano, methali 'Asiyesikia la mkuu huvunjika guu', msemo 'Mdomo huponza kichwa', nahau 'Ana mkono mrefu' inamaanisha mwizi, kitendawili 'Anakukodolea macho lakini hakujui' jibu lake ni picha, msimu 'mguu wa bia' kumaanisha mguu mzuri, na shirikina 'Ukikata kucha kwa meno utakuwa fukara'.

Lengo la makala hii ni kujadili mambo (maudhui) yanayozungumziwa na semi zinazotaja viungo vya mwili pamoja na dhima, mchango au nafasi ya semi hizo kwa jamii. Kutokana na ukubwa wa utanzu wa semi makala hii itamakinikia aina mbili tu za semi ambazo ni methali na misemo ya Kiswahili. Methali ni semi fupifupi za kimapokeo zenye

* Idara ya Fasihi, Mawasiliano na Uchapishaji, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, E-mail: shaniom@yahoo.co.uk , shaniom@udsm.ac.tz

kuelezea fikra, maarifa, hekima na mafunzo yanayotokana na uzoefu wa jamii fulani (Matei 2011). Kuhusiana na misemo inafasiliwa kwamba ni aina ya semi fupi zenye maana fiche zinazokubalika na kutumiwa kueleza au kufafanua ukweli na hekima kwa jamii (Ngure 2003). Misemo ni kipengele cha semi inayotumia lugha ambayo si ya moja kwa moja ambayo huwa na mvuto maalumu kwa wasomaji (Mng'aruthi 2008). Hivyo, methali na misemo hueleza jambo fulani kwa ufupi kwa kutumia mbinu mbalimbali za lugha kama vile lugha ya picha, mafumbo, sitiari na ishara (taz. Mauya 2008, Bianco na Emig, 2009, Wamitila 2012, Simiyu 2011, King'ei na Ndalu 2016 na Salla 2017a, 2017b).

Utanzu wa semi, kupitia vipera vyake mbalimbali, umetafitiwa na wataalamu mbalimbali duniani kote. Mathalani, Schipper (2006) amekusanya methali kutoka katika jamii na lugha mbalimbali duniani ili kulinganisha na kulinganua namna mwanamke anavyosawiriwa katika methali hizo. Mieder (2008, 2014) amekusanya na kuchunguza methali katika nyuga mbalimbali kama vile sanaa, utamaduni, sanaajadiya, historia, fasihi na vyombo vya habari kutoka Uingereza na Marekani na kufafanua dhima zake katika maisha. Pia, amechunguza kuhusu methali za kisasa, maendeleo na mwelekeo wake. Tafiti nyingine, hususani kwa upande wa Afrika, zimefanywa na Finnegan (2012) kupitia utafiti wake wa fasihi simulizi katika Afrika. Pia, utafiti kama vile wa Momoh (2000) umechunguza falsafa katika methali za Afrika. Naye Hussein (2009) amechunguza ulinganinishi wa dhima, hadhi na utambulisho wa masuala ya wanawake katika methali kutoka Ethiopia, Sudani na Kenya. Tafiti zote hizi ni muhimu katika kutanabahisha na kuendeleza utanzu wa semi katika lugha za jamii mbalimbali.

Kwa upande wa semi za Kiswahili tafiti kadhaa zimefanyika (taz. Mlacha 1985, Badru 2019, Mgogo 2020, Maitaria 2022) pamoja na kukusanya semi hizo na kuzitolea fasiri na matumizi yake katika jamii (taz. Mauya 2008, Bianco na Emig 2009, Wamitila 2012, King'ei na Ndalu 2016 na Salla 2017a, 2017b). Tafiti nyingine zilizofanyika zinahusu semi katika matini mbalimbali za Kiswahili kama vile vazi la kanga na nafasi yake kiutamaduni na kijamii (Beck 2005, Zawawi 2005), vyombo vya usafiri (Mturo 2011, Omari 2011a, Ponera na Kikula 2017, Mchepange 2021), muziki (Omari 2011b), na katika makawa na vipepeo (Omari, Mkomwa na Mlingi 2016). Nao Mchepange na Mahenge (2022) wamechunguza mitazamo mbalimbali inayobebwa na methali za Kiswahili zinazohusu ulemavu, na Mberwa (2024) amechunguza masuala ya kifantansia yanayojitokeza katika misemo ya kiitikadi ya Kiswahili katika jamii ya Wazanzibari.

Licha ya utanzu huu kujadiliwa na wanazuoni mbalimbali, bado usawiri wa viungo vya mwili katika semi haujachunguzwa bayana. Kwa mantiki hiyo, makala hii inalenga kuchunguza semi kuhusu viungo vya mwili na nafasi yake katika jamii. Data za utafiti huu zilikusanywa kwa njia ya usomaji wa nyaraka mbalimbali kuhusu semi katika machapisho kutoka maktabani (kama vile, Mauya 2008, Bianco na Emig 2009, Wamitila 2012, King'ei na Ndalu 2016 na Salla 2017a, 2017b) na mtandaoni[1]. Makala hii imegawika katika sehemu kuu nne: sehemu ya kwanza ni utangulizi unaohusiana na lengo la utafiti, kazi tangulizi kuhusu semi, na mbinu za ukusanyaji data. Sehemu ya pili ni uwasilishaji na uchambuzi wa data. Sehemu hii inafuatiwa na sehemu ya tatu ambayo inahusu mjadala, na sehemu ya nne ni hitimisho.

## Uwasilishaji na Uchambuzi wa Data

Semi za Kiswahili takribani mia mbili zinazohusu viungo vya mwili zilikusanywa kutoka katika methali, misemo, misimu, vitendawili, nahau, na shirikina kutoka maktabani na mtandaoni. Kama ilivyoelezwa hapo awali makala hii itajikita katika data kutoka katika aina mbili tu za semi, ambazo ni methali na misemo (taz. Kiambatisho). Uchambuzi wa

[1] https://mhariri.com/kamusi/learn-swahili/proverbs-in-swahili-and-their-translations-and-meanings/, https://swahiliproverbs.afrst.illinois.edu/index.htm

semi hizo umefanywa kwa kuzingatia maana halisi ya semi hizo, na maana zilizokusudiwa katika muktadha mpana wa kijamii. Hii inatokana na kwamba methali huwa zina maana ya nje na maana ya ndani (Schipper, 2006, Madumulla, 2001).

**Maudhui na Dhima za Semi Zinazozungumzia Viungo vya Mwili**

Utafiti umebaini kwamba katika lugha ya Kiswahili, semi zinazotaja viungo vya mwili huzungumzia masuala mbalimbali. Masuala hayo ni pamoja na umuhimu wa viungo hivyo, kufanya kazi, kauli nzuri na usiri, umoja na ushirikiano, mapenzi, malezi, kifo, na tabia za binadamu. Masuala hayo yanasawiri utamaduni wa jamii husika na huwalenga wanajamii wakubwa kwa wadogo. Semi hizo zina dhima mbalimbali kwa jamii na zimetumia mbinu mbalimbali za lugha kama vile tamathali za semi kwa mfano picha, ishara, sitiari, tashihisi na tashibiha katika kuwasilisha maudhui yake. Mjadala wa malengo hayo ni kama ifuatavyo:

Mwili wa binadamu umeumbwa na viungo mbalimbali na kila kiungo kina kazi yake kisayansi hata kijamii. Semi hizo zinasawiri kuhusu umuhimu wa viungo mbalimbali na nafasi yake kwa kiumbe na jamii pana inayohusika. Semi zifuatazo zinagusia suala hili:

1 Dira ya binadamu ni kichwa.
2 Halla halla mti na macho.
3 Heri kufa macho kuliko kufa moyo.
4 Asiyesikia la mguu huvunjika guu.
5 Kilimo ni uti wa mgongo.
6 Heri kujikwaa mguu/kidole kuliko kujikwaa ulimi.
7 Athari ya kidole hasara ya mwili.
8 Aliyeruka shimo kaagana na nyonga.
9 Mdharau mwiba mguu huota tende.
10 Kidole chako kibaya sikikate.

Usemi “Dira ya binadamu ni kichwa” unalenga kueleza umuhimu wa kichwa kwa binadamu hasa ikizingatiwa kwamba ndani yake kuna ubongo ambao unahusika na masuala ya akili, kumbukumbu, kufikiri na kufanya maamuzi mbalimbali katika maisha. Hivyo kichwa/akili huongoza maisha, hivyo ni dira. Kwa upande wake methali “Halla halla mti na macho” inahusu kufanya jambo kwa umakini na uangalifu. Kiungo macho na mti vinapokaribiana inaonesha athari inayoweza kutokea iwapo mti utaingia machoni, kiumbe kinaweza kupoteza uwezo wa kuona, na kurudisha nyuma utendaji wa mambo yake mbalimbali katika jamii. Hivyo ni vema kuyalinda macho kwa umakini na kufanya mambo kwa uangalifu. Kwa ujumla methali hii inashauri kuwa waangalifu katika utendaji wa mambo mbalimbali. Pamoja na umuhimu wa macho methali nyingine inashauri kwamba “Heri kufa macho kuliko kufa moyo”. Kinachosisitizwa hapa ni kwamba ingawa macho ni muhimu (yanatuwezesha kuona) lakini moyo ni muhimu zaidi. Moyo hufanya kazi kama vile kusukuma damu na kusafisha damu hivyo ukisimama tu kufanya kazi husababisha kifo. Hivyo, ni sawa na kusema kwamba ni afadhali mtu kukosa uwezo wa kuona kuliko kukosa uhai wa kuishi. Vilevile, katika methali hii suala la kutokata tamaa (kutokufa moyo) linahimizwa. Moyo, pamoja na kazi yake ya msingi ya kusukuma damu mwilini, unahusishwa na imani na matumaini. Unapokuwa na moyo wa kufanya kazi na kutenda, hata kama macho yamekufa, unaweza kujiletea maendeleo.

Umuhimu wa viungo vya mwili unaonekana pia kupitia methali “Asiyesikia la mkuu huvunjika guu” na “Ng’ombe akiumia mguu hurejea zizini”. Methali ya kwanza inaonesha umuhimu wa mguu kwa kuonya kwa vitisho kwamba asiyesikia kufanya jambo fulani basi mguu wake utavunjika. Methali ya pili inaonesha hali anayoipata kiumbe (ng’ombe) aliyevunjika mguu akiwa malishoni kwamba inabidi kurejea nyumbani (zizini). Methali hizi kwa ujumla zinaonesha umuhimu wa viungo hivyo kwa kiumbe kwamba atashindwa kutembea na kufanikisha shughuli zake mbalimbali.

Kadhalika, methali “Heri kujikwaa mguu/kidole kuliko kujikwaa ulimi” inaeleza kwamba maumivu ya ulimi ni makali kuliko ya mguu au kidole. Hii inatokana na madhara yanayoweza kutokea kwa mtu iwapo viungo hivyo vikiumia. Hivyo, ulimi (maneno) unapewa uzito zaidi kwani unaweza kusababisha athari kubwa pale unapoumia/kukosea kusema kuliko athari zinazoweza kupatikana kwa kujikwaa/kuumia mguu au kidole. Athari ya kukosea kusema inaweza kuwaathiri wanajamii wengine na hata kuweza kuleta mfarakano na kutoelewana katika jamii. Kadhalika, msemo “Kilimo ni uti wa mgongo” unalenga kuonesha nafasi ya kilimo kwa uchumi na maendeleo ya jamii. Uti wa mgongo ni kiungo kinachoshikilia mwili mzima, kinasaidia kiumbe kusimama, kujongea, kupata umbo husika, na kusaidia mawasiliano kati ya ubongo na mwili. Kilimo kinahusishwa na uti wa mgongo kutokana na kwamba uti wa mgongo ni kiungo muhimu katika mwili wa binadamu kama ilivyo kilimo kwa maendeleo ya kiuchumi ya nchi. Msemo huu ulikuwa maarufu sana nchini Tanzania baada ya kupata uhuru mnamo miaka ya 1960. Mathalani, kwa upande wa siasa na uchumi Mwalimu Julius Nyerere, Rais wa kwanza wa Tanzania, alitambua kilimo ni muhimu kwa Taifa na alihamasisha kwa kauli mbalimbali kama vile “Siasa ni kilimo” na “Kilimo ni uti wa mgongo” (Msuya 2022). Hivyo, kilimo kilipewa aula ili kuletea maendeleo kwa Taifa. Nao msemo “Athari ya kidole hasara ya mwili” unaonesha umuhimu wa kila kiungo katika mwili kwani viungo vinategemeana na kuathiriana kiutendaji wake. Hivyo maumivu ya kidole kimoja huweza kuhisika, kusambaa na kuathiri mwili mzima. Kwa maana pana zaidi inaweza kusemwa kwamba jambo dogo linaweza kuathiri watu wengine. Kwa ujumla, semi zote hizi zinaonesha thamani ya viungo mbalimbali vya mwili na haja ya kuvitunza ili visiharibike na kuathiri utenda kazi wa kiumbe husika. Hivyo, kuna haja ya kulinda viungo na afya za miili yetu ili kuepusha madhara yatakayojitokeza. Kwa kuhusisha thamani ya viungo husika semi hizi hushauri, hukanya au kuonya mtu kuhusu hatari ya kutozingatia au kufanya jambo fulani.

Umuhimu wa viungo vya mwili na haja ya kuvitunza au kuvitumia kwa umakini na uangalifu linajitokeza pia kupitia methali “Aliyeruka shimo kaagana na nyonga”. Nyonga ni mfupa/sehemu iliyopo kati ya kiuno na paja. Methali hii inamtaka mtu kujihadhari anapotaka kufanya jambo la hatari; awe ametafakari madhara yake kabla ya kutenda. Hii ni kutokana na kwamba kwa mfano mtu anayeruka shimo anaweza kuteguka nyonga na kumletea maumivu au hata ulemavu. Uangalifu na umakini wa kuvilinda viungo vya mwili ili kuepusha madhara unadhihirika pia katika methali “Mdharau mwiba mguu huota tende”. Methali inaelekeza kwamba ni muhimu kulitatua jambo likiwa bado dogo ili kuepuka hatari na matatizo makubwa yanayoweza kumkuta mtu baadaye. Nayo methali “Kidole chako kibaya sikikate” inahimiza kuhusu umuhimu wa viungo hivyo na kunasihi kwamba tusidharau vitu tulivyonavyo, tuvilinde kwani vina manufaa. Hata kama mtu anahisi kiungo chake fulani ni kibaya kuna siku kitakuja kumfaa. Katika muktadha mpana methali hii inasisitiza kutowadharau ndugu na jamaa hata kama wana kasoro fulani za kimwili, kiakili au wana sifa au tabia mbaya, huwa wana manufaa yao (Wamitila 2012).

Umuhimu wa kufanya kazi kwa binadamu ni suala mojawapo linalodhihirika katika semi hizi. Methali za Kiswahili zinahimiza wazi suala la ufanyaji kazi katika jamii (Maitaria 2022). Kazi ndio msingi wa maisha na ndio humtofautisha binadamu na mnyama. Suala la umuhimu wa kufanya kazi limeoneshwa kwenye semi mbalimbali kupitia viungo kama mkono, mguu, moyo, na tumbo kama ifuatavyo:

11 Aliyepeleka mkono kutamalaki si kazi.
12 Mguu uliotoka Mtume kauombea.
13 Mguu mtembezi haukosi mwiba.
14 Heri ya kufa macho kuliko kufa moyo.
15 Ngoja ngoja yaumiza matumbo.
16 Tumbo ni mzigo wa mwenyewe.

Kazi ni msingi wa maendeleo na ni kipimo cha utu. Semi hizi zinaeleza kwamba penye juhudi huwa kuna mafanikio na mapato, hivyo “Aliyepeleka mkono kutamalaki si kazi”. Inamaanisha kwamba anayefanya kazi kwa bidii hupata kwa urahisi na hufanikiwa.

Hivyo, mtu anahimizwa kutoka kwenda kujishughulisha kwani “Mguu uliotoka Mtume kauombea”. Suala la mtu kutoka nyumbani kwenda nje ama shambani, ofisini au kwengineko kufanya jambo fulani jema linahalalishwa kupitia dini au imani za jamii. Mathalani, Usilamu na Ukristu ni dini kubwa miongoni mwa jamii za Waafrika (Mbiti 1969) ikiwemo Waswahili, nao Mitume ni watumishi wa Mungu kupitia dini hizo. Suala la kutoka linafungamanishwa na imani ya dini na hivyo kuleta ari na matumaini ya mafanikio kwa mtendaji. Hata hivyo angalizo linatolewa kwamba mtu anayetoka nyumbani kwake njiani huweza kukanyaga miba, kwa maana ya kukutana na vikwazo au changamoto, kwani “Mguu mtembezi haukosi mwiba”. Hivyo, mbali na jitihada hizo pia kuna changamoto japo kidogo. Zaidi hamasa inatolewa ya kutokata tamaa katika kutafuta riziki kwani “Heri ya kufa macho kuliko kufa moyo”. Inashauriwa kwamba ni afadhali mtu kukosa uwezo wa kuona (kufa macho) kuliko moyo kuacha kufanya kazi (moyo kufa). Hivyo, methali inamaanisha kwamba ni heri macho kukosa uwezo wa kuona (kufa macho) kuliko moyo kukata tamaa (kufa moyo) kwani kukata tamaa kunapoteza ari ya mtu kufanya kazi. Suala ambalo si zuri kwani kufanya kazi kuna faida kadhaa ikiwemo kuimarika kisaikolojia, kupata ujuzi na mali ambazo husaidia katika maendeleo ya nyanja nyingine mbalimbali (De Klerk, Nel & Koekemoer 2015).

Suala la kuchukua hatua mara moja katika ufanyaji kazi pia linasisitizwa. Mambo yafanywe bila kuchelewa kwani “Ngoja ngoja huumiza matumbo.” Kufanya kazi huondoa umasikini na husaidia kukabiliana na maisha na kuleta maendeleo ya jamii. Kadhalika, inasisitizwa kila mmoja kuwajibika katika kufanya kazi yeye mwenyewe kwani “Tumbo ni mzigo wa mwenyewe.” Kila mtu anawajibika kutafuta riziki mwenyewe ili kuleta tija kwake, kwa jamii na Taifa. Kwa ujumla semi hizi zinasisitiza binadamu kujishughulisha kufanya kazi, mbali na changamoto zake, ili kujiletea maendeleo.

Suala la heshima na tabia njema kwa wakubwa na watu wenye mamlaka limezungumziwa katika methali hizi, kama ifuatavyo:

17 Asiyeonywa huonywa na macho yake.
18 Asiyesikia la mkuu huvunjika guu.
19 Masikio hayapiti kichwa.
20 Chanda chema huvikwa pete.

Heshima na tabia njema ni masuala muhimu ya kimaadili ambayo yanazungumziwa kupitia semi hizi. Methali “Asiyeonywa huonywa na macho yake” inasisitiza haja ya mtu kuzingatia mafundisho na ushauri kutoka kwa wakubwa wake. Kushindwa kufanya hivyo kunaweza kumsababishia madhara au kukutana na changamoto katika safari ya maisha yake. Nayo methali “Asiyesikia la mkuu huvunjika guu” inahusu haja ya kusikiliza na kufuata ushauri na maneno ya wazazi au wakubwa ili kuepuka matatizo katika maisha. Kimsingi methali hizi zinatumia lugha ya vitisho kwamba mtu ambaye ni mkaidi kuonywa au kuelekezwa basi ‘ataonywa na macho yake’ au ‘atavunjika mguu’. Lengo la methali hizi ni kusisitiza umuhimu wa kusikiliza wakuu au watu wenye uzoefu ili kuepuka matatizo. Vilevile, methali ya “Masikio hayapiti kichwa” inasisitiza pia adabu, utii na heshima kwa wakubwa au mamlaka. Si vizuri kwa mtu kujiona ana busara na hekima kuliko watu waliomzidi umri au viongozi wake, daima sikio ni dogo kuliko kichwa. Hivyo, ni vema kutambua nafasi za watu ambao wako juu yako kiumri au kiutawala. Nayo, methali “Chanda chema huvikwa pete” inaangazia watu wenye sifa nzuri, tabia na maadili mema na kuona kwamba wanapaswa kutuzwa ili kutambua mchango wao na kuwa mfano wa kuigwa. ‘Tabia njema humuwezesha mtu kukubalika kijamii, kuwa na manufaa na kuwa mwenye tija’ (Stark 2018: 897). Kwa ujumla semi hizi zinasisitiza ujenzi wa maadili mema katika jamii kwa kuhimiza vijana na watoto kuwa na heshima kwa wakubwa na mwenendo mwema katika jamii.

Kuchunga kauli tunazotoa na kuficha siri kwa mambo ambayo hayana ulazima kutoka nje na kujulikana na watu ni mambo ya msingi ili kujenga jamii yenye maelewano na maadili. Semi zifuatazo zinasawiri suala hili:

21 Sikio halilali na njaa.

22 Macho hayana pazia.

23 Moyo wa mtu ni msitu wa giza.

24 Mtu siri husema na moyo wake.

25 Shingo hubeba vyombo, moyo hubeba mambo.

26 Heri kujikwaa mguu/kidole kuliko kujikwaa ulimi.

27 Ulimi unauma kuliko kisu.

28 Mtu huchongewa na ulimi wake.

Semi hizi kuhusu viungo kama sikio, macho, moyo, ulimi na shingo zimetumia lugha iliyojaa tashihisi, sitiari na picha ili kubainisha sifa na kazi ya viungo hivyo na kuwasilisha maudhui yanayohusika. Kwa mfano, sikio limepewa sifa ya kutolala na njaa kwa maana kwamba daima husikia mambo yanayoongelewa. Macho yanaonekana kukosa pazia ya kuyazuia kumaanisha kwamba yanaona kila kitu kinachopita mbele yake; kiwe cha stara au cha aibu. Aidha, moyo wa mtu ni msitu kumaanisha kwamba unaficha siri na mambo mengi bila kuonekana. Ni vigumu kujua mawazo yaliyo kwa binadamu wenzetu mpaka wayaseme. Hivyo kama mtu ana siri au jambo lake ni vema afiche moyoni mwake "Mtu siri huficha moyoni mwake" kwani moyo hubeba mambo mengi tofauti na shingo ambayo hubeba vyombo. Hivyo, tusiseme mambo ambayo hatutaki watu wayajue wala tusiyaoneshe mambo ambayo hatutaki watu wayaone.

Kadhalika, ulimi nao unaonekana ni kiungo kinachoweza kuleta madhara kwa msemaji kama hakikutumiwa vizuri katika kutoa kauli zake. Madhara yake ni makubwa, ni afadhali uumie au ujikwae mguu au kidole kuliko kukosea kwenye kauli zako au kusema mambo ovyo ovyo. Kuzungumza ndiyo ada ya mja katika maisha yetu ya kila siku, hata hivyo hatupaswi kuongea kila wakati. Kudhibiti ulimi wetu kwa kutosema mambo yetu na mambo ya siri ya wengine ni jambo jema na la busara. Maneno (ulimi) mabaya yanaweza kuwa na athari na madhara makubwa kuliko kuumizwa mwili na kifaa kama kisu. Kwa ujumla, semi zote zinaonesha haja ya kuficha siri, matendo au mambo yetu yenye umuhimu na faragha ili yasisikike au kuonekana na watu wengine kama hakuna ulazima. Binadamu anatahadharishwa kuchunga kauli zake (ulimi) na kuhifadhi mambo yake moyoni ili kuepuka madhara yanayoweza kujitokeza. Msemo maarufu wa Kiswahili unadhihirisha kwamba "Mdomo huweza kuponza kichwa". Ni vema kusema maneno ambayo hasa umeyakusudia na yanayofaa, kwani ulimi wako unaweza kukudhuru na kukusababishia maafa.

Umoja na ushirikiano ni nguzo ya jamii katika utendaji au utekelezaji wa masuala mbalimbali. Waafrika huthamini sana umoja na mshikamano katika kukamilisha masuala mbalimbali ya jamii (Mulokozi 2017). Semi kuhusu suala hili zinabainika kupitia data za utafiti huu kama inavyodhihirika hapa:

29 Mkono mmoja haulei mtoto/mwana.

30 Kidole kimoja hakivunji chawa.

31 Macho mengi huona kuliko moja.

32 Mkono utoao ndio upatao.

Suala la umoja linasisitizwa sana katika jamii ya Waswahili na ya Waafrika kwa ujumla. Methali za Kiafrika kupitia falsafa ya Ubuntu zinasisitiza sana suala la umoja na ushirikiano, badala ya utengano, ili kuleta maendeleo ya kweli kwa jamii (Thakhathi & Netshitangani, 2020). Methali hizi zinasisitiza umuhimu wa umoja, ushirikiano, na mshikamano wa kijamii katika nyanja mbalimbali za maisha ya binadamu. Ushirikiano unahitajika kwa mfano katika malezi ya mtoto. Suala la malezi si la mama, baba au familia tu bali ni la jamii nzima (Msigala, 2024), hivyo, "Mkono mmoja haulei mtoto/mwana". Pia, ushirikiano unahimizwa katika kufanya kazi nyingine mbalimbali kwani "Kidole kimoja hakivunji chawa". Mafanikio huja kwa haraka na ufanisi kama watu wanashirikiana katika

shughuli zao. Aidha, kushauriana na kufanya maamuzi au mambo mbalimbali kwa pamoja ni jambo zuri kwani "Macho mengi huona kuliko moja". Kwa kufanya hivyo husaidia kurekebisha kasoro zitakazojitokeza kwa urahisi. Vilevile, suala la kutoa na kuwasaidia wengine ni jambo la msingi na la kiutu, kwa kufanya hivi jamii husaidiana na kuimarisha uhusiano wao. Hivyo, msemo kama "Mkono utoao ndio upatao" unahimiza ukarimu, kusaidiana na kujaliana miongoni mwa wanajamii. Mtu anayetoa kuwasaidia wengine inaaminika kwamba hupata zaidi. Kinachobainika katika semi hizi ni kwamba jitihada za pamoja na ushirikiano katika shughuli mbalimbali ili kujiletea mafanikio ni jambo la msingi katika maisha ya binadamu.

Kifo ni faradhi kwa kila binadamu nacho hakikuachwa kuzungumziwa katika semi hizi zinazohusu viungo vya mwili. Mifano ifuatayo inadhihirisha:

33 Kifo ki karibu, ki kisogoni mwako.
34 Kufa kwa mdomo mate kutawanyika.
35 Kufa kwa mkundu mavi kutawanyika.
36 Kuregarega si kufa, kufa ni kuoza utumbo.
37 Heri ya kufa macho kuliko kufa moyo.
38 Sikio la kufa halisikii dawa.

Semi hizi zote katika maana yake ya msingi zinaelezea kifo. Kupitia viungo vya mwili kama vile macho, moyo, kisogo, mdomo, sikio na mkundu suala la kufa limezungumziwa ingawa kwa namna tofauti. Kwa kuanza na "Kifo ki karibu, ki kisogoni mwako" inaonyesha kuwa kifo ni sehemu ya maisha yetu na kipo karibu sana nasi. Tunaishi nacho na kinatufuata kila tuendapo. Methali hii inamkumbusha binadamu kujiandaa na kifo kwani kinaweza kutokea saa na wakati wowote. Mbali na hilo methali "Kufa kwa mdomo mate kutawanyika" na "Kufa kwa mkundu mavi kutawanyika" zinaonesha namna kufa kwa mdomo na mkundu kunavyosababisha kutawanyika kwa mate na mavi. Suala la kijamii linaloelezwa hapa ni kwamba kifo huleta athari na madhara kwa wanajamii wanaobaki. Suala hili linasawiriwa kisitiari ambapo mdomo na mkundu inaweza kuwakilisha wazee/wazazi/walezi au viongozi na mate na mavi inaweza kumaanisha watoto/wategemezi/wanaoongozwa. Kufa kwao kunasababisha kuharibika kwa masuala mbalimbali kwani wao ndio wanachukuliwa kuwa wasimamizi wa familia na washauri wa masuala mbalimbali katika jamii. Hivyo kufa kwao kunaweza kuleta changamoto za kifedha kwa familia, kushindwa kujisimamia na kujiongoza, na kufarakana katika usimamizi na uendeshaji wa masuala yao ya kifamilia au kitaasisi.

Methali "Kuregarega si kufa, kufa ni kuoza utumbo" inaeleza kwamba mtu hujihesabu kuwa amekufa baada ya kuoza, si kwa kudhoofika kiafya au ugonjwa kwani unaweza kupona au kurejea katika hali yako ya kawaida. Kwa mapana yake methali inasisitiza mtu kutokata tamaa pale anapokuwa amedhoofika au kuwa dhaifu kutokana na sababu mbalimbali kwani kudhoofika/kulegalega si sawa na kufa bali mpaka pale utakapoona umeoza utumbo kabisa. Utumbo kama kiungo muhimu katika masuala ya chakula unapooza ndipo unaweza kujihesabu kuwa umekufa. Mtu aendelee kupambana na changamoto zinazomfika ili ajikwamue. Suala la kifo pia linaongelewa kupitia macho na moyo katika "Heri ya kufa macho kuliko kufa moyo". Methali hii inamaanisha kwamba ni heri kupoteza uwezo wa kuona (kufa macho) kuliko kupoteza matumaini na kukata tamaa ya kufanya jambo (kufa moyo), hata hivyo fasiri yake ya kawaida ni kwamba ni afadhali kupoteza macho kuliko kupoteza uhai (mapigo ya moyo kusimama kufanya kazi), yaani kufa. Hivyo basi, kuishi ni kuzuri kuliko kufa. Aidha, falsafa ya Kiafrika inaamini kwamba kifo si mwisho wa kuwapo kwa mtu bali ni mwanzo wa maisha mengine ya mwanadamu katika ulimwengu wa wafu hai ambao huendelea kuwasiliana pia kukumbukwa na walio hai kwa namna mbalimbali (Mbiti 1975). Nayo methali "Sikio la kufa halisikii dawa" inaweza kufasiriwa kwa namna mbalimbali. Katika muktadha wa malezi na ushauri

inaweza kufasriwa kwamba mtu ambaye hataki kubadilika hata kama akishauriwa na kuelekezwa kiasi gani hawezi kamwe kubadilika. Aidha, katika muktadha wa kifo tunaweza kusema kwamba mtu kama siku yake ya kufa imefika hata kama zikifanyika jitihada kiasi gani za kuokoa uhai wake hawezi kupona. Atakufa tu.

Kifo huenda pamoja na kuzaliwa au uzazi. Hata hivyo, suala la uzazi halijabainika wazi kupitia data za utafiti huu zinazohusu semi za viungo vya mwili. Mathalani, ipo methali “Mficha uchi hazai” ingawa haijataja kwa umahususi kiungo kipi hasa cha ‘uchi’. Kwa mujibu wa TUKI (2019) uchi (pia tupu) ni kiungo cha binadamu kama vile kuma, mboo na mkundu. Maoni yangu ni kwamba limetumika neno ‘uchi’ kutokana na mtazamo miongoni mwa Waafrika kuhusu unyeti wa viungo vya sehemu za siri, kwamba havipaswi kutajwa hadharani. Methali hii imetumika kumaanisha mtu anapaswa kusema yanayomsibu katika maisha ili aweze kusaidiwa. Ukificha tatizo au jambo fulani ni vigumu kupata suluhisho lake kutoka kwa jamii. Mtu akiwa na shida aseme asione aibu ili apate msaada. Sawa na ambavyo kama unaficha uchi na kuona aibu kwa mwenzi wako suala la kujamiiana linakuwa gumu, hivyo kushindwa kupata watoto, yaani kuzaa. Akichunguza ukiushi wa kaida za lugha katika methali za Kiswahili, Mgogo (2020) anaeleza kwamba methali za Kiswahili zinazotaja viungo vya mwili vya siri zimekiuka maadili ya jamiilugha ya Waswahili kwa sababu viungo hivyo ni mwiko kutamkwa hadharani. Jamii nyingi za Kiafrika hazitamki wazi viungo vya mwili vinavyohusishwa na ngono au sehemu za siri. Inapaswa kutumia tafsida. Miongoni mwa methali anazobainisha ni “Nguo ya kuazima haisitiri matako” na “Nyani haoni kundule, huliona la mwenzie”.

Malezi ya watoto ni mambo ya msingi katika jamii ili kupata kizazi chema na jamii yenye maadili yanayotakiwa. Suala hili linajitokeza katika semi kadhaa ikiwemo zifuatazo:

39 Mwana hufuata kisogo cha nina.

40 Mkono mmoja haulei mtoto/mwana.

41 Kiganya alichonyia mwana huoshwa hakikatwi.

42 Asiyesikia la mkuu huvunjika guu.

Methali zina dhima kubwa katika malezi ya watoto, vijana na jamii kwa ujumla (Mlacha 1985, Maitaria 2022). Katika methali “Mwana hufuata kisogo cha nina” nafasi ya mama (nina) katika kuathiri na kujenga tabia ya mtoto inaelezwa. Mtoto anasawiriwa kuwa ni kiumbe ambacho hujifunza tabia na mambo mbalimbali kwa kufuata au kuiga yale anayotenda mzazi wake, hasa mama. Mama anapewa nafasi kutokana na kwamba ukuaji na malezi ya mtoto unajitokeza kabla na baada ya kuzaliwa kwa mtoto. Kwa kuwa mtoto hufuata tabia ya mzazi, hususani mama, ushauri unatolewa kwa wazazi kuwa na matendo ya kuigwa ili jamii iwe na kizazi chenye maadili mema. Nayo methali “Mkono mmoja haulei mtoto/mwana” inaeleza malezi ya mtoto yanavyopaswa kuhusisha jamii pana. Jukumu la kulea mtoto si la mtu mmoja, kama vile mzazi. Malezi ya mtoto ili yawe na mafanikio yanahitaji ushirikiano kutoka kwa watu wengine wa ndani na nje ya familia. Miongoni mwao ni ndugu, marafiki na asasi za kijamii kama vile shule na asasi za dini. Aidha, methali “Kiganya alichonyia mwana huoshwa hakikatwi” inazungumzia malezi hasa kwa kumlenga mzazi, mlezi au jamii. Suala linalosisitizwa hapa ni kwamba kulea mwana ni jukumu zito hivyo kunahitajika busara, upendo, uvumilivu na huruma. Inashauriwa kwamba mtoto akifanya makosa (kunyia kiganja) azidi kuelekezwa zaidi na kwa busara (kuosha kiganja) badala ya kuchukua hatua kali sana (kukata kiganja) kwa makosa aliyofanya. Elimu inatolewa kwa wazazi na walezi ili kuepusha madhara ambayo yangeweza kutokea kwa mtoto pindi hatua kali sana zikichukuliwa dhidi yake kutokana na makosa anayofanya. Kwa upande wake methali “Asiyesikia la mkuu huvunjika guu” inahusu malezi lakini hasa kwa kumlenga mtoto ambaye anaonekana kutozingatia mafundisho, ushauri na maelekezo ya mzazi, mlezi au mkuu wake ambao ndio wenye uzoefu wa kimaisha. Tahadhari inatolewa kwake kwamba iwapo hazingatii mafunzo hayo

anaweza kuharibikiwa katika maisha yake. Ni muhimu watoto na vijana kufuata ushauri wa wazazi au watu waliowazidi umri ili kufanikiwa maishani. Maadili ni muhimu kuzingatia kama mwongozo katika kuongoza utendaji wa jambo lolote (Koskinen & Pokorn, 2020).

Mapenzi na upendo baina ya wenzi au jamii yanazungumzwa vema katika semi kuhusu viungo vya mwili. Baadhi ya semi hizo hueleza kwamba:

43 Asili ya huba, mwanzowe ni jicho.
44 Mapenzi hayana macho.
45 Moyo hauna subira.
46 Moyo wa kupenda hausemezeki.
47 Moyo wa kupenda na kuwiza huwa.
48 Moyo mbaya haukai na nyumba.

Kwa kuanza na methali “Asili ya huba, mwanzowe ni jicho” inaeleza nafasi ya jicho katika kuona na kuvutiwa na kitu. Hivyo, mapenzi huanza baada ya macho kuona na kuvutiwa na kitu au mtu, bila kujali ubaya, udhaifu au kasoro ya kitu hicho. Pia inaelezwa kwamba “Mapenzi hayana macho” kwa maana kwamba mwenye kupenda haoni kasoro au hila ya kitu ingawa macho anayo. Bendi ya DDC Mlimani Park waliwahi kuimba kwamba ‘Mtu chake apendacho, hakina hila machoni. Huridhika kuwa nacho japo hakina thamani’. Kimsingi macho na moyo hutegemeana katika kujenga hisia zake za mapenzi. Baada ya macho kuona moyo unachukua nafasi yake ya kupenda kiasi hata cha kushindwa kujizuia. Methali “Moyo hauna subira” na “Moyo wa kupenda hausemezeki” zinadhihirisha suala hili. Mtu akipenda kitu au mtu huwa hasikilizi maneno ya watu, hata ukiwa ni ushauri wa kufaa kiasi gani. Moyo unakuwa hauna muda wa kujadiliana tena, kwani umeshaamua kupenda. Suala jingine ni kuhusu upendo kwa jamii. Methali “Moyo mbaya haukai na nyumba” unahimiza jamii kuacha chuki, wivu, na kuwa na uhusiano mzuri na jamaa zetu. Nyumba ambayo watu wake wana roho mbaya si ajabu kukuta inakimbiwa na ndugu na jamaa, kwani hukosa upendo na amani.

Vitu huwa vina pande mbili zinazopingana (de Saussure, 1916, Lévi-Strauss 1955), mathalani chenye mwanzo kina mwisho, giza kinyume chake ni nuru na mwanamke kinyume chake ni mwanaume. Hivyo basi, mapenzi nayo huweza kubadilika na kuwa chuki. Mapenzi huisha, hakuna mapenzi ya milele. Hivyo, methali “Moyo wa kupenda na kuwiza huwa” inamaanisha kwamba moyo unaopenda unaweza pia kuchukia au kuacha kupenda kitu ambacho hapo awali ilikuwa inakipenda sana. Ndio maana unaweza ukasikia kwamba watu wapendanao ndio wagombanao.

Binadamu hujengwa na tabia, nazo huweza kumtofautisha kati yake na mwingine au kati yake na mnyama. Baadhi ya tabia hizo zimezungumziwa kupitia semi hizi kuhusu viungo vya mwili kama inavyooneshwa hapa:

49 Nyani haoni kundule, huliona la mwenziwe.
50 Aliyekula kitovu chako, hatakuachia utumbo.
51 Aliyekusoza chanda kukupiga sio kazi.
52 Aliyekwelekeza chanda aweza kukupiga kofi.

Methali “Nyani haoni kundule, huliona la mwenziwe” inaeleza jinsi binadamu ambaye anafananishwa na nyani kwa kawaida hawezi kuona udhaifu na makosa yake (kundule) bali huona makosa, udhaifu na kasoro za watu wengine. Methali inaonesha ugumu wa binadamu kutambua makosa yake lakini yu rahisi kutambua makosa ya wenzake. Nazo methali “Aliyekula kitovu chako hatakuachia utumbo”, “Aliyekusoza chanda kukupiga sio kazi” na “Aliyekwelekeza chanda aweza kukupiga kofi” kwa ujumla zinaeleza tabia ya binadamu kwamba akianza kukufanyia jambo baya dogo basi hashindwi kukufanyia jambo baya kubwa. Tahadhari inatolewa kwamba kama mtu amekufanyia ubaya au uovu fulani basi anaweza kufanya ubaya na uovu mkubwa zaidi hata kuweza kukuangamiza, yaani “Aliyekula kitovu chako, hatakuachia utumbo”. Hivyo,

tusidharau watu waliowahi kutufanyia uovu na mambo mabaya wakati fulani kuwa wanaweza kutufanyia ubaya kwa siku zijazo. Kupitia methali hizi jamii inapewa tahadhari na kuwa waangalifu na kutambua tabia hizi za binadamu na athari zake kwao ili kujiandaa na kukabiliana nazo.

**Mjadala kuhusu Semi husika**

Semi za viungo vya mwili, kwa kutumia wahusika mbalimbali kama vile wanyama na binadamu, zimewasilisha vizuri maudhui na dhima mbalimbali. Semi hizo zimechanganya tajiriba za binadamu na maarifa ya kisayansi kuhusiana na viungo hivyo. Mathalani, moyo umehusishwa na hisia, ujasiri na usiri, miguu na mikono imehushiwa na kufanya na kutenda kazi mbalimbali, ulimi umehusishwa na kauli na uaminifu, masikio na macho yamehusishwa na umakini na udadisi, na kichwa kimehusishwa na kumbukumbu, akili na hekima. Hivyo, semi hizi zimesawiri ukweli fulani wa maisha na kuwasilisha vema maudhui na mafundisho yaliyotarajiwa kwa jamii. Maudhui katika semi hizi hayahusu tu kuzungumzia viungo hivyo bali huhusu muktadha mpana wa kijamii na kiutamaduni. Hivyo, mambo yanayojadiliwa na semi hizo yanahusu umuhimu wa viungo hivyo, ufanyaji kazi katika jamii, malezi, mapenzi, kifo, uzazi, maadili, na kauli nzuri. Maudhui ya semi hizi yanalenga makundi mbalimbali wakiwemo watoto, wazazi au walezi na jamii kwa ujumla. Methali ni hazina ambayo imejaa imani, mawazo na busara za kijadi na taarifa kuhusu dini na falsafa ya jamii mbalimbali za Kiafrika (Mbiti, 1975). Wabantu huamini katika kuheshimu wakubwa kwani huwa na maarifa, ujuzi na uzoefu wa mambo. Wakubwa huwa na uwezo wa kuwasiliana na wahenga. Kupitia semi, falsafa ya Kiafrika inadhihirika bayana, kama inavyoelezwa na Mbiti kwamba falsafa ya Kiafrika ni uelewa, mawazo, mantiki na mtazamo ya jinsi Waafrika wanavyofikiri, kutenda au kuzungumza katika miktadha mbalimbali ya maisha (Mbiti 1975). Masuala hayo ni kuhusu utu, upendo, heshima kwa wakubwa na mamlaka na umoja na ushirikiano katika kufanya mambo mbalimbali katika jamii kama vile katika malezi ya watoto (Mkono mmoja haulei mtoto/mwana) na kufanya kazi (Kidole kimoja hakivunji chawa).

Semi, kama zilivyo kazi nyingine za fasihi, zina mchango mkubwa kwa jamii na ni nyenzo muhimu ya kutolea elimu katika jamii. Semi hizi hushauri na hukanya kuhusu tabia fulani ili jamii kuwa na watu wema au kuepuka jambo fulani baya. Mathalani, zinahimiza kutunza viungo vya mwili ili kuwa na afya njema. Zinashauri kushirikiana katika kufanya mambo kama vile malezi ya watoto na kufanya kazi kwa bidii ili kujiletea maendeleo. Pia zinashauri kutokata tamaa katika kufanya jambo au unapopatwa maradhi au changamoto fulani.

Kwa mfano, kuhusu malezi na maadili katika jamii, wazazi na walezi wameelekezwa na kushauriwa kuhusu nafasi yao katika malezi ya watoto wao kwamba wanapaswa kutumia busara na hekima (Kiganya alichonyia mwana huoshwa hakikatwi) pia kushirikiana ili kupata watoto wenye tabia njema. Kadhalika, watoto wamehimizwa kuzingatia mafundisho kutoka kwa wakubwa wao ili kuwa na maadili na maisha mema (Asiyesikia la mkuu huvunjika guu). Waafrika, wakiwemo Waswahili, huamini katika heshima kwa mababu na wazee (Kezilahabi, 1985). Semi hizi zinaelimisha kuhusu ujenzi wa maadili mema katika jamii kwa kuhimiza vijana na watoto kuwa na heshima kwa wakubwa na mwenendo mwema katika jamii. Maadili yanayohimizwa ni kauli nzuri, utunzaji wa siri, tabia njema, upendo, umuhimu wa umoja, ushirikiano, na mshikamano wa kijamii katika nyanja mbalimbali za maisha ya binadamu. Hivyo, semi hizi zimetoa elimu kuhusu maadili mbalimbali katika jamii. Hivyo, “kwa Waafrika, methali huchukuliwa kama urithi wa kiutamaduni unaozingatiwa sana kutokana na imani kwamba zimefumbata falsafa, busara na maarifa ya jamii” (Balogun, 2006: 87). Aidha, semi hizi zinaelekeza jamii haja ya kujikinga au kujiepusha na madhara na hatari mbalimbali inayoweza kutokea kutokana na kufanya au kutokuzingatia kitu fulani. Hili linajitokeza katika semi kama

“Asiyesikia la mkuu huvunjika guu”, “Heri kujikwaa kidole/mguu kuliko kujikwaa ulimi. Methali nyingine ni zile zinazohusu kutahadharisha kuhusu tabia za binadamu za kuweza kumdhuru binadamu mwingine kama vile “Aliyekula kitovu chako, hatakuachia utumbo”.

Aidha, semi hizi hutahadharisha na kuonya mtu kuhusu hatari ya kutozingatia au kufanya jambo fulani. Kutafakari kabla ya kutenda jambo, kutatua jambo mapema kabla halijawa kubwa ili kuepuka hatari na matatizo makubwa yanayoweza kumkuta mtu baadaye. Pia jamii inapewa tahadhari na kuwa waangalifu na kutambua tabia mbaya, ovu na hila za binadamu wengine ili kujiandaa na kukabiliana nazo. Zinanasihi kuhusu uzazi na kifo kama vile umuhimu wake kwa jamii, changamoto zinazoweza kujitokeza na namna ya kukabiliana nazo. Kwa ujumla, semi husika zimesheheni maadili mbalimbali yenye kulenga kumlea, kumwongoza na kumwelekeza binadamu kwenye misingi bora ya maisha (Mlacha, 1985, Maitaria 2022).

**Hitimisho**

Makala hii ilihusu kuchunguza semi za Kiswahili kuhusu viungo vya mwili na nafasi yake kwa jamii. Lengo kubwa la kuchunguza semi kuhusu viungo vya mwili ni kubaini mambo yanayozungumziwa pamoja na mchango wa semi hizo katika jamii. Semi mbalimbali zimechunguzwa na kubainika kwamba zinazungumzia masuala mbalimbali kuhusu viungo husika na kuhusu jamii pana. Kupitia kwayo masuala mbalimbali yamesawiriwa ikiwemo umuhimu wa kufanya kazi, umoja na ushirikiano, heshima, tabia njema, malezi na kutunza siri. Masuala mengine ni kifo, mapenzi, uangalifu na umakini katika masuala mbalimbali. Semi hizo ni muhimu sana kwa jamii inayohusika kwani hufanya kazi ya kurithisha amali za jamii, kuelimisha, kuendeleza falsafa ya Kiafrika, kuonya, na kushauri. Kupitia semi hizi jamii hupata uelewa wa masuala mbalimbali yenye manufaa kwa jamii.

**Marejeleo**


Badru, Z. A. (2019). Dhima ya taswira katika ufasiri na uteguzi wa vitendawili. *Kioo cha Lugha*, 17, 179-198.

Balogun, O. A. (2006). A Jurisprudential analysis of Yoruba proverbs. *The Cambrian Law Review*. 37, 86-97.

Beck, R. M. (2005). Texts on textiles: Proverbiality as characteristic of equivocal communication at the east African coast (Swahili). *Journal of African Cultural Studies*, 17(2), 131-160.

Bianco, C.D. & Emig, J. (eds.) (2009). *Diwani ya methali: An anthology of proverbs in Kiswahili*. Vienna Department of African Studies University of Vienna.

De Klerk, M., Nel, J.A. & Koekemoer, E. (2015). Work-to family enrichment:Influences of work resources, work engagement and satisfaction among employees within the South African context, *Journal of Psychology in Africa*, 25:6, 537-546, DOI: 10.1080/14330237.2015.1124606

de Saussure, F. (1916). *Course in general linguistics*. Duckworth.

Finnegan, R. (2012). *Oral literature in Africa*. Open Book Publishers CIC Ltd.

Hussein, J. W. (2009). A discursive representation of women in sample proverbs from Ethiopia, Sudan, and Kenya. *Research in African Literatures*, 40(3), 96-108.

Kezilahabi, E. (1985) African philosophy and the problem of literary interpretation. University of Wisconsin-Madison.

King’ei, K. & Ndalu, A. (2016). *Kamusi ya Semi za Kiswahili*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Koskinen, K. and Nike K. P. (2020). Ethics and translation: An introduction. *The Routledge Handbook of Translation and Ethics*, 1-10. https://www.routledgehandbooks.com/doi/10.4324/9781003127970-1

Lévi-Strauss, C. (1955). The structural study of myth. *The Journal of American Folklore*, 68(270), 428-444.
Madumulla, J.S. (2001). Proverbs: A pack of lies? UTAFITI, 4, 257-74.
Maitaria, J.N. (2022). Matumizi ya methali za Kiswahili kwa jamii: Mifano kutoka nchini Kenya. *Kioo cha Lugha*, 20(1): 1-17. DOI: http://doi.org/10.56279/KL/20.i.1
Matei, A.K. (2011). Fani ya fasihi simulizi kwa shule za upili. Nairobi: Oxford University Press.
Mauya, A.B. 2008. *Semi: Maana na matumizi*. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.
Mberwa, A.R. (2024). Fantasia katika misemo ya kiitikadi ya jamii ya Wazanzibari. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA).
Mbiti, J.S. (1969). *African religion and philosophy*. London: Heinemann Educational Books Ltd.
Mbiti, J.S. (1975). *Introduction to African religion*. London: Heinemann Educational Books Ltd.
Mchepange, S.O. (2021). Usawiri kijinsia wa dhamira katika misemo ya kwenye vyombo vya usafiri nchini Tanzania na dhima zake kwa jamii. *Kioo cha Lugha*, 19(1), 161-179.
Mchepange, S.O. & Mahenge, E.G. (2022). Methali za Kiswahili zihusuzo ulemavu: Mitazamo na athari zake katika jamii. *Swahili Forum*, 29, 114-133.
Mgogo, C.P. (2020). Methali za Kiswahili hukwepa ukiushi wa kaida za lugha. *Ruaha Journal of Arts and Social Science* (RUJASS), 6(1), 73-89.
Mieder, W. (2008). *Proverbs speak louder than words: Folk wisdom in art, culture, folklore, history, literature and mass media*. Peter Lang Publishing, Inc.
Mieder, W. (2014). Futuristic paremiography and paremiology: A plea for the collection and study of modern proverbs. *Folklore Fellows' Network*, 44, 13-17, 20-24.
Mlacha, S.A.K. (1985). Dhima ya methali katika malezi. *Kiswahili*, 52(1), 175-186.
Mng'aruthi, T. K. (2008). *Fasihi simulizi na utamaduni*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.
Momoh, C.S. (2000). *Philosophy in African proverbs*. African Philosophy Projects Publications.
Msigala, S.H. (2024). Uchunguzi wa mkengeuko wa malezi kwahusika katika riwaya teule za Kiswahili. Tazmili ya PhD Kiswahili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
Msuya, E. (2022). Nyerere na ukombozi. *Mwananchi,* Aprili 21, 2022. https://www.mwananchi.co.tz/mw/habari/kitaifa/nyerere-na-ukombozi-3790062
Mturo, N.G. (2011). Dhima ya semi zilizoandikwa kwenye daladala: Uchambuzi wa vipengele vya lugha na dhamira. Tasnifu ya MA Kiswahili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
Mulokozi, M. M. (2017). *Utangulizi wa fasihi ya Kiswahili*. KAUTTU Ltd.
Ngure, A. (2003). Fasihi simulizi ya shule ya sekondari. Nairobi: Phoenix Publishers Limited.
Omari, S. (2011a). Poetics of daladala: The Case of HIV/AIDS dialogue in daladala ticket slogans. *Kiswahili*, 74:78-94.
Omari, S. (2011b). The role of slang in understanding bongo flava content and culture. In Imani Sanga & Mitchel Strumpf (Eds.), *Readings in Ethnomusicology* (pp. 159-172). Dar es Salaam University Press.
Omari, S., Mkomwa, A. and Mlingi, S. (2016). Texts on Swahili cultural artefacts in Tanzania and the representation of women's voice'. *JULACE*, 1(1), 131-150.
Ponera, A. S. & Kikula, I. S. (2017). *Misemo ya vyombo vya usafiri*. Afroplus Industries Limited.
Salla, H.D. (2017). *Vitendawili vya Kwetu* (1). Dar es Salaam: African Proper Education Network.

Salla, H.D. (2017). *Nahau za Kwetu* (1). Dar es Salaam: African Proper Education Network.

Schipper, M. (2006). *Never marry a woman with big feet: women in proverbs from around the world*. Amsterdam University Press.

Stark, L. (2018). Early marriage and cultural constructions of adulthood in two slums in Dar es Salaam, *Culture, Health & Sexuality*, 20(8), 888–901 https://doi.org/10.1080/13691058.2017.1390162.

Simiyu, W. F. (2011). *Kitovu cha fasihi simulizi*. Mwanza: Serengeti Bookshop.

Thakhathi, A. & Netshitangani T. G. (2020). Ubuntu-as-Unity: Indigenous African proverbs as a 're-educating' tool for embodied social cohesion and sustainable development, *African Identities*, 18:4, 407-420, DOI: 10.1080/14725843.2020.1776592

TUKI. (2019). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.

Wamitila, K. (2012). *Kamusi ya Methali* (Toleo Jipya). Nairobi: Longhorn Publishers.

Zawawi, S. (2005). *Kanga, the cloth that speaks*. Azania Hills Press.

**Kiambatisho: Semi (Methali na Misemo)**

| Na. | Semi |
|---|---|
| 1. | Ajabu ya shingo kukataa kulala kitandani/chini. |
| 2. | Akili ni nywele kila mtu ana zake. |
| 3. | Akosaye (titi) la mama hata la mbwa huamwa (hunyonya). |
| 4. | Akupaye kisogo sio mwenzio. |
| 5. | Aliyekula kitovu chako, hatakuachia utumbo. |
| 6. | Aliyekusoza chanda kukupiga sio kazi. |
| 7. | Aliyekwelekeza chanda aweza kukupiga kofi. |
| 8. | Aliyepeleka mkono kutamalaki si kazi. |
| 9. | Aliyeruka shimo kaagana na nyonga. |
| 10. | Amejifunga kwa ulimi wake. |
| 11. | Asiyeonywa huonywa na macho yake. |
| 12. | Asiyesikia la mkuu huvunjika guu |
| 13. | Athari ya kidole hasara ya mwili. |
| 14. | Bora kujikwaa dole kuliko ulimi. |
| 15. | Chanda chema huvikwa pete. |
| 16. | Dira ya binadamu ni kichwa. |
| 17. | Doa usoni huonekana kwa kioo. |
| 18. | Furaha ya mwenye meno mwenye mapengo hacheki. |
| 19. | Halla halla mti na macho. |
| 20. | Heri kujikwaa guu/dole kuliko kujikwaa ulimi. |
| 21. | Heri ya kufa macho kuliko kufa moyo. |
| 22. | Ila ya kwapa kunuka pasipo kidonda. |
| 23. | Jino la pembe si dawa ya pengo. |
| 24. | Kata pua uunge wajihi. |
| 25. | Kichwa cha kuku hakistahili kilemba. |
| 26. | Kichwa cha nyoka hakibandikwi mtungi. |
| 27. | Kichwa ni shajara. |
| 28. | Kidole chako kibaya chaweza kufaa siku mbaya. |
| 29. | Kidole chako kibaya sikikate. |
| 30. | Kidole chema huvishwa pete |
| 31. | Kidole kimoja hakivunji chawa. |
| 32. | Kidole kimoja kikiuma vingine vyatoa damu. |
| 33. | Kifo ki karibu, ki kisogoni mwako. |
| 34. | Kiganya alichonyea mwana huoshwa hakikatwi. |
| 35. | Kufa kwa mdomo mate kutawanyika. |

36. Kufa kwa mkundu mavi kutawanyika.
37. Kuku mgeni hakosi kamba mguuni.
38. Kunguru mwoga hukimbiza mbawa zake.
39. Kuregarega si kufa, kufa ni kuoza utumbo.
40. Lililo moyoni ulimi huiba.
41. Macho hayana pazia.
42. Macho mengi huona kuliko moja.
43. Macho yaliyoiona milima hayashtuki mabonde.
44. Maneno matupu/makali hayavunji mfupa.
45. Mapenzi hayana macho.
46. Masikio hayapiti kichwa.
47. Mbawala mwoga hukimbiza pembe zake.
48. Mdomo huponza kichwa.
49. Mdomo siri ya gunda.
50. Mdomo ukila pua haitaki.
51. Meno ya mbwa hayaumani.
52. Mficha uchi hazai.
53. Mgeni ni (ki)pofu ingawa ana macho.
54. Mguu mtembezi haukosi mwiba.
55. Mguu ukikanyaga mavi haukatwi.
56. Mkia wa nyani haumbanduki nyani.
57. Mkono mmoja haubebi/haulei mtoto/mwana.
58. Mkono mmoja hauchinji ng’ombe.
59. Mkono mtupu haulambwi.
60. Mkono uliotia jiwe majini ule ule utaopoa.
61. Mkono usioweza kuukata ubusu.
62. Mkono utoao ndio upatao.
63. Mkono wako ukichafuka, huukati.
64. Mnywa maji kwa mkono mmoja kiu yake i pale pale.
65. Moyo hauna subira.
66. Moyo hujua uchungu wa nafsi yake.
67. Moyo huona mbali kuliko kichwa.
68. Moyo mbaya haukai na nyumba.
69. Moyo ni chuo.
70. Moyo ni kilindi.
71. Moyo ni nyongo, ukigeuka udongo.
72. Moyo safi silaha ya kutosha.
73. Moyo ukitamani utashawishika.
74. Moyo wa kupenda hauna mithali [mithili].
75. Moyo wa kupenda hausemezeki.
76. Moyo wa kupenda na kuwiza huwa.
77. Moyo wa mtu ni msitu wa giza.
78. Moyo wa mwenzako ni tundu la chupa.
79. Moyo wa mwenzio tundu ya mwanzi hauingiliki.
80. Mpa mgongo (kisogo) si mwenzio.
81. Mpiga ngumi ukuta huumiza mkonowe.
82. Mpiga mbizi nchi kavu huupunjua usowe.
83. Mtembezi hula miguu yake
84. Mtoto akibebwa hutazama kisogo cha nina.
85. Mtu huchongewa na ulimi wake.
86. Mtu siri husema na moyo wake.
87. Mwana akinyea kiweo hakikatwi.
88. Mwana hufuata kisogo cha nina.
89. Mwenye macho haambiwi tazama.
90. Mwenye moyo wa kuonywa huonywa.

91. Mwenye tende hana paja.
92. Mwenye tumbo ni tumbole angafunga mkaja.
93. Mwungwana hanuni mashavu, hununa moyoni.
94. Ndovu hashindwi na pembeze/mkongawe.
95. Ng’ombe haelemewi na nunduye.
96. Ngoja ngoja huumiza matumbo.
97. Nguo ya kuazima haisitiri matako.
98. Nyama ya ulimi tamu.
99. Nyani haoni kundule, huliona la mwenziwe.
100. Shingo hubeba vyombo, moyo hubeba mambo.
101. Si kila mwenye makucha huwa simba.
102. Sikio halilali na njaa.
103. Sikio halipiti kichwa.
104. Sikio la kufa halisikii dawa.
105. Titi la mama li tamu jingine haliishi hamu.
106. Tumbo ni mzigo wa mwenyewe.
107. Ufukara hufanya mtu awe na udhalili moyoni.
108. Uji moto haupozwi kwa nch ya ulimi.
109. Ukibebwa usilevyelevye miguu.
110. Ukienda kwa chongo funga lako jicho.
111. Ukitaka riba sikio ziba.
112. Ukiiga tembo kunya utapasuka msamba.
113. Ukubwa wa pua si wingi wa kamasi.
114. Ulimi hauna mfupa.
115. Ulimi huuma kuliko meno.
116. Ulimi upanga.
117. Umasikini ni ngozi.
118. Umekula ng’ombe mzima washindwa na mkia?
119. Upeo wa macho si mwisho wa dunia.
120. Usicheze na simba ukamtia mkono kinywani.
121. Usikaange mbuyu ukawaachia wenye meno watafune.
122. Vita havina macho.

Recebido em: 23/02/2025
Aceito em: 24/06/2025

**Para citar este texto (ABNT):** MCHEPANGE, Shani Omari. Semi za Kiswahili kuhusu Viungo vya Mwili na Nafasi yake kwa Jamii. *Njinga & Sepé:* Revista Internacional de Culturas, Línguas Africanas e Brasileiras. São Francisco do Conde (BA), vol.5, nº Especial II, p. 65-79, jul./dez.2025.

**Para citar este texto (APA):** Mchepange, Shani Omari (jul./dez.2025). Semi za Kiswahili kuhusu Viungo vya Mwili na Nafasi yake kwa Jamii. *Njinga & Sepé: Revista Internacional de Culturas, Línguas Africanas e Brasileiras.* São Francisco do Conde (BA), 5 (Especial II): 65-79.